

Lugha ya

Fikranet Connect Book Series

MUNGU

Nyakati za Mateso



MAKUSUDI 5 YA MUNGU
KUHUSU MAUMIVU
TUNAYOYAPITIA

Dickson John

Author | Coach | Trainer | Speaker

JE, MUNGU HUZUNG'MZA TUWAPO KATIKA MATESO

MANUFAA YA KITABU

Najua umesoma vitabu vingi na kuna mambo ambayo umejifunza kutokana na vitabu hivyo, name pia nimejifunza mambo mengi kupitia vitabu. Lakini kusoma vitabu vingi haimanishi ni ukomo wa maarifa ama fikra, bado tunayo nafasi nyingi ya kujifunza hata kama tumewahi kujifunza.

Kitabu hiki ni mfulululizo wa vitabu vifupi kutoka Fikranet Connect vilivyojaa madini na nondo za kutosha kukusaidia wakati wa mahitaji. Hakilengi kuharibu dini yako, bali kimeelezewa katika mtazamo wa Kimungu, kwa mujibu wa imani ya Kikristo.

Kitabu hiki ni kitabu cha aina yake, kwa kuwa hakijasimulia hadithi na mtindo wa maisha ya mtu kama vile wengi wafanyavyo, mwandishi amenuia kukuandikia wewe ili kuyalinganisha maisha yako na wewe mwenyewe kuliko kujilinganisha na wengine.

Kitabu hiki kimesheheni madini ya kutosha kama inavyoainishwa hapa chini:-

1. Utangulizi

Hapa utapata mwongozo na kusudio la kitabu kizima, na namna unavyoweza kukikosama.

2. Usishuke Thamani.

Utatiwa moyo katika sura hii na kwamba hupaswi kujidharau wala kujikatisha tamaa kwa kile unachopitia. Na kwamba ile thamani yako ya msingi ya utu inapaswa kubaki ikiwa imara na asiwepo mtu, kitu, hali au ugumu wowote unaopaswa kukufanya kushuka thamani.

3. Lugha 4 za Mungu nyakati za mateso.
Mungu hajakaa kimya katika hali yako uliyonayo sasa, yamkini unapitia ugumu fulani katika mambo mbalimbali, unapaswa kutambua kuwa Mungu anafahamu hali na hadhi yako kwa sasa. Kuna jambo Mungu analisema, na unapaswa kulisikiliza ili uweze kustahimili katika hali ngumu.
4. Kusudio la Mungu,
Katika sura hii itatiwa moyo kwa kujua makusudi matano (5) ya Mungu kuhusu majaribu, changamoto, matatizo na nyakati ngumu katika Maisha.
5. Tafakuri
Katika sehemu hii ya mwisho utajifunza baadhi ya tafakuri na mitazamo unayopaswa kuwa nayo unapokumbana na hali ngumu katika maisha.

Pamoja na kitabu hiki, unaweza kupata vitabu vingine kutoka Fikranet Connect, mpaka sasa tuna vitabu hivi:-

- i. Fanikisha ndoto yako.
- ii. Una nini Mkononi?
- iii. Unaweza Inuka Tena.
- iv. Maaamuzi yenye ufanisi.

Dickson John

+255 (0) 714 585 455

+255 (0) 766 545 583

dicksonjohn04@gmail.com